HALMASHAURI YA MJI WA TARIME

SHULE YA SEKONDARI NKONGORE,
S.L.P 78,
TARIME.

Tarehe _____

Kumb Na.NKGR/SS/TTC/REG/5237/

JINA LA MWANAFUNZI _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA JANUARI 2022

I. UTANGULIZI:

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza Januari 2022 katika Shule ya Sekondari Nkongore. Shule ya Sekondari Nkongore ipo Mtaa wa Kwigoronto, Kata ya Ketare, Halmashauri ya Mji wa Tarime na pia shule hii ipo umbali wa kilometa nane (8) toka Tarime Mjini mwelekeo wa Mlima Chambiri.

Ili ufike Nkongore Sekondari panda bodaboda ambazo zinazopatikana karibu na uwanja wa mpira wa Serengeti. Shule itafunguliwa tarehe 17/01/2022, saa moja asubuhi na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 17/01/2022 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/01/2022, ni shule ya kutwa.

II. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

SARE ZA SHULE.

a) Suruali mbili kwa wavulana yenye mikunjo **(turn up)moja** ya rangi ya **dark green** mifuko mitatu na marinda mbili lakini isiwe (modo) na pili rangi **nyeusi,** mwanafunzi atakayekuja na suruali ya modo **atalazimika kushona iliyo bora**
b) Mkanda mweusi kwa wavulana wenye chuma cha kawaida na siyo vinginevyo.
c) Sketi mbili kwa wasichana rangi ya **dark green moja na na nyeusi moja** marinda box sita (6), sketi iwe ndefu kuvuka goti na pindo la tumbo lisizidi **SM 5,** sketi fupi hazitaruhusiwa kamwe, mwanafunzi atakayekuja na sketi fupi **atalazimika kushona inayofaa**
d) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi kwa wavulana na wasichana.
e) Sweta **dark green na dark bluu** kwa ajili ya baridi kwa wavulana na wasichana**.**
f) Soksi nyeusi ndefu jozi mbili (2) kwa wavulana.
g) Soski nyeupe ndefu hadi kwenye magoti jozi mbili (2) kwa wasichana
h) Viatu vyeusi vyenye kufungwa na kwamba na visivyo na visigino virefu kwa wavulana na wasichana.

i) Raba za michezo rangi nyeusi
j) Track suti ya rangi nyeusi yenye michirizi meupe pembeni kwa ajili ya michezo
k) T- shirt na nembo kwenye sare ya shule utapata maelekezo hapa shuleni

MAHITAJI YA DARASANI

i. Kalamu
ii. Mkebe (mathematical set) wa mahesabu.
iii. Madaftari tisa (9) conter book Q2
iv. Begi la kubebea madaftari
v. Uje na folder file (faili) moja lenye kamba kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake.

***NB**. Wanafunzi wasichana wa **KISLAMU** watavaa sketi za malibda box sita (6) ndefu zisizobana zinazofunika miguu na shati nyeupe na **Hijabu** ya kichwani nyeupe.*

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Nmaba 25 ya Mwaka 1978 na ilivyolekebishwa kwa sheria namba kumi (10) ya mwaka 1995, na pia shule inazingatia miongozo na sare zote zinazotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Taknolojia yenye Dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais Tamisemi yenye jukumu la kusimamia na kuendesha Eimu Nchini.

III. SHERIA NA KANUNI ZA KUZINGATIA

a) Mwanafunzi anatakiwa kuwahesimu viongozi wa kitaifa, wazazi, walimu na wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzake na jamii inayo izunguka shule kwa ujumla.
b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vye masomo ya darasani na nje ya darasani kulingana na ratiba ya shule.
c) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni na kufanya shughuli zote atakazopewa walimu wake wa masomo, zamu na darasa bila kukosa.
d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya kazi zote za darasani hasa home work na kazi mradi.
e) Mwanafunzi anatakiwa kuwepo shuleni muda wote wa masomo na asivuke eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu.
f) Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi wake wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule muda wote akiwepo shuleni.

IV. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

i. Wizi wa mali ya umma/ wanafunzi wenzake

ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Matumizi ya madawa ya kulevye kama vile uvutaji wa bangi, mirungi, marujuani na ulevi wa pombe.
v. Kupiga au kupigana.
vi. Kuharibu mali za umma kwa maksudi
vii. Kudharau bendera ya Taifa. Mwenge wa Uhuru na Wimbo wa Taifa.
viii. Kupata au kusababisha mimba
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kutoa mimba
xi. Kumiliki simu ya mkononi

KIPENGELE HIKI KIJAZWE NA MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI.

Mimi …… mzazi/ mlezi wa mwanafunzi …….. wa kidato cha kwanza 2022 ninakiri kuwa nimezisoma na kuzielea sheria na kanuni zilizoelekezwa na uongozi wa shule, na ninaahidi kwamba mwanagu atazifuata kikamilifu kwa kipindi chote cha masomo yake.

Saini ya mzazi/mlezi ……. Tarehe……

V. VIAMBATANISHO

a) Kiambatanisho “A” kijazwe na mganga baada ya mwanafunzi kupimwa.
b) Kimbatanisho “B” lete photocopy ya cheti cha kuzaliwa mara tu shule inapofunguliwa

Nakutakia maandalizi mema

KARIBU NKONGORE
ELIMU NI HAZINA

……..
Johannes B.Oyolla
Mkuu wa Shule.

To the Doctor concerned

RE: **MEDICAL EXAMINATION FORM**

Please examine the following student and furnish me current health status requested by school Authority

NAME .....

ANDRESS.....

OCCUPATION .....

Age ..... Height (in cm) ..... weight .....

1. GENERAL EXAMINATION
    i. Ears .....
    ii. Eyes.....
    iii. Skin .....
    iv. Upper &lower extremities .....
    v. Chest .....
    vi. Abdomen .....
    vii. Dental .....
2. PAST MEDICAL HISTORY
3. LABARATORY EXAMINATION
    i. Urinalysis .....
    ii. Stool .....
    iii. Sputum .....
    iv. Bs .....
    v. Widal test .....
    vi. U.P.T Test .....

Remarks .....

.....

.....

Date .....

Name ..... Title ..... Signature .....